

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Pili - Tarehe 3 Aprili, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, leo ni Kikao cha Pili cha Mkutano wa Kumi na Tano, tunaendelea. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

SPIKA: Hati za kuwasilishwa Mezani, Ofisi ya Waziri Mkuu, tafadhali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:-

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

Toleo Na. 04 la tarehe 25 Januari, 2019;
Toleo Na. 05 la tarehe 01 Februari, 2019;
Toleo Na. 06 la tarehe 08 Februari, 2019;
Toleo Na. 07 la tarehe 15 Februari, 2019;
Toleo Na. 08 la tarehe 22 Februari, 2019;

Toleo Na. 09 la tarehe 01 Machi, 2019;
Toleo Na. 10 la tarehe 08 Machi, 2019;
Toleo Na. 11 la tarehe 15 Machi, 2019; na
Toleo Na. 12 la tarehe 22 Machi, 2019.

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha, 2019/2020.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali leo tunaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum Mbunge wa Solwa. Kwa niaba yake, ahsante nakuruhusu.

Na. 9

Ahadi ya Ujenzi wa Vituo Viwili vya Afya – Solwa

MHE. EZEKIEL M. MAIGE (K.n.y. MHE. AHMED A. SALUM)
aliuliza:-

Waziri Mkuu alipofanya ziara katika Mkoa wa Shinyanga aliahidi ujenzi wa Vituo viwili vya Afya katika Jimbo la Solwa

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo lililoulizwa kwa niaba ya Mheshimiwa Salum na Mheshimiwa Magolyo Maige Ezekiel, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 inayoelekeza kuwa na Kituo cha Afya kila Kata sambamba na utekelezaji wa ahadi mbalimbali za viongozi wa Kitaifa. Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga yenye Jimbo la Solwa ilipewa kipaumbele na kutengewa shilingi milioni 900.0 kwa ajili ujenzi na ukarabati wa Kituo cha afya Tinde, kilichogharimu shilingi milioni 400 na Kituo cha Afya Samuye kilichogharimu shilingi milioni 500. Vituo hivyo vimekamilika na vimeanza kutoa huduma kwa wananchi.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ni miongoni mwa Halmashauri 67 zilizoidhinishwa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri. Fedha zote zimepokelewa na ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Ahmed Ally Salum Mbunge wa Solwa kuwa ahadi za viongozi zitaendelea kutekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

SPIKA: Mheshimiwa Ezekiel Maige, nimekuona.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona na kunipa nafasi, lakini pia naomba nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu hayo, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza; Mheshimiwa Waziri Mkuu pia alifanya ziara katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala na kwa kuona hali ilivyokuwa na hasa wananchi walivyojitolea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano katika kukabiliana tatizo la afya, alikubali pia kutushika mkono kwa kutupatia shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Isaka. Nataka kufahamu ni hatua gani imefikiwa katika utekelezaji wa ahadi hiyo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu?

Swali la pili; kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba kuna Halmashauri 67 ambazo zimepatiwa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi kwa Hospitali za Wilaya, kwa bahati mbaya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala haina hospitali ya Wilaya na haiko katika hizi Halmashauri 67. Nataka kufahamu: Je, itawezekana sasa kwa awamu hii ambayo itakuwa ni ya pili mwaka 2019/2020 Halmashauri hii nayo ikatengewa hiyo fedha ili na yenyewe iweze kupata Hospitali ya Wilaya? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI Mheshimiwa Joseph Sinkamba Kandege, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, kipekee kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Maige na wananchi wake jinsi ambavyo wamekuwa wakijitolea katika suala zima la afya, wamejenga maboma mengi kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu ametembelea Msalala na akahaidi kwamba na Kituo cha Afya Isaka nacho kingeweza kupatiwa fedha; ni ukweli usiopingika kwamba Isaka ni miongoni mwa eneo ambalo lina watu wengi na iko haja ya kuhakikisha kwamba kunakuwa na Kituo cha Afya ili kupunguza adha ya wananchi wengi kupata huduma ya afya. Naomba aendelee kuiamini Serikali kama ambavyo nimejibu katika swali langu la msingi kwamba kwa kadri fursa ya fedha inapokatikana ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba ahadi zote za viongozi wa Kitaifa tunazitekeleza. Nasi bado tunakumbuka hiyo ahadi, naomba Mheshimiwa Maige avute subira.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kwamba katika Halmashauri 67, Halmashauri yake haikuwa miongoni mwa zile ambazo zilipata fursa ya kujengewa hospitali. Sina uhakika katika orodha ya hivi sasa hivi tuna jumla ya Halmashauri 27 ambazo katika bajeti, tutakapokuja kuomba fedha tutaenda

kuongeza fedha katika Halmashauri nyingine 27. Tuombe Mungu katika hizo 27 na yake iwe miongoni mwake.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na swali la pili la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, kwa niaba yake.

Na. 10

Kudhibiti Watoto Wanaobeba Mizigo Hapa Nchini

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM (K.n.y. MHE. MGENI JADI KADIKA) aliuliza:-

Katika baadhi ya maeneo hapa nchini ikiwemo Dodoma wapo watoto ambao hutoa huduma ya kubeba mizigo na kupewa ujira mdogo. Kutokana na kufanya kazi hizo ni wazi wanakosa haki za msingi kama elimu na malezi bora.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuondoa tatizo hilo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo. Bado tupo TAMISEMI, Naibu Waziri, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huduma za ulinzi wa mtoto zinatekelezwa kupitia Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009. Katika kusimamia utekelezaji wa Sheria hiyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto ulioanza kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2021/2022. Tathmini imebaini kuwa watoto wengi wanaojihusisha

na kazi za kubeba mizigo masokoni ni matokeo ya umasikini uliokithiri kwa baadhi ya kaya, kuondokewa na wazazi wao kwa maambukizi ya UKIMWI, migogoro ya ndoa na ukatili dhidi ya watoto.

Mheshimiwa Spika, mkakati unaotekelezwa na Serikali ni kutoa elimu kwa jamii kuhusu haki za msingi za mtoto kupata elimu na malezi bora. Aidha, utoaji wa elimu bila malipo umetoa fursa kwa watoto wengi wenye umri wa kwenda shule kuandikishwa kuanza elimu ya awali kupitia mfumo rasmi na mfumo usio rasmi. Vilevile, mradi wa *TASAF* umewezesha kuzitambua kaya za watoto walio katika mazingira hatarishi na kuzisaidia kiuchumi ili ziweze kumudu mahitaji ya kaya zao kwa kuwapatia watoto mahitaji ya msingi ikiwemo elimu na afya.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa wito kwa wazazi kutimiza wajibu wao wa kuwalea na kuwatunza watoto ikiwemo kuwapa fursa ya elimu. Aidha, jamii inao wajibu wa kushirikiana na wazazi kuwatunza na kuwalinda watoto ambao ni Taifa la kesho kwa kutowatumikisha katika kazi ambazo haziendani na umri wao. Serikali haitasita kuchukua hatua kwa vitendo vyovyote vya unyanyasaji wa watoto vinavyokiuka Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009.

SPIKA: Mheshimiwa Mosoud, kwa niaba ya Mheshimiwa Mgeni.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake kwa swali la msingi la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, nataka niwahakikishie tu kwamba bado kuna ongezeko kubwa la watoto hawa katika Barabara ya Sita, Barabara ya Tisa hapa Dodoma na katika Soko la Dodoma la Matunda na Mboga Mboga.

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie kwamba hali hii Jiji la Dodoma wanaifahamu. Sasa utuambia mwarobaini au mkakati madhubuti ama mkakati mahususi wa kuweza

kuwasaidia watoto hawa, kwa sababu kila siku ongezeko hili kidogo linatisha.

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba baadhi ya watoto hawa wazazi wao tayari wamefariki kwa maradhi mbalimbali, lakini kuna baadhi ya watoto hawa wazazi wao wako hai na wako katika maeneo ya karibu katika maeneo mbalimbali. Sasa wanasema kwamba watatoa elimu, atuambie mkakati wa ziada kuhakikisha kwamba wale watoto ambao wazazi wao wapo hai wanachukua hatua gani ya dharura kuhakikisha wazazi hawa wanapatikana na suala hili kulikomesha?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, kwanza suala kwamba kuna ongezeko, hiyo inakuwa kidogo ni *relative term*, kwa sababu ongezeko hilo unalipima kuanzia lini? Kama nilivyojibu katika swali langu la msingi, kwa mujibu wa sheria ni wajibu kuhakikisha kwamba mtoto analelewa katika mazingira mazuri. Jitihada zimefanywa na Serikali kwanza kuwatambua hawa watoto.

Kwa mfano, kwa Mkoa wa Dodoma na hasa Jiji la Dodoma, jitihada za makusudi zimefanyika kwanza kuhakikisha kwamba wale watoto ambao wana wazazi wao wanarudishwa na kuunganishwa na familia kwa sababu wajibu wa kwanza wa kumlea mtoto ni wa familia.

Mheshimiwa Spika, kuna *cases* kama ambazo watoto wanalazimika kuondoka katika mazingira na kwenda katika mazingira hayo kwa sababu aidha, wameondokewa na wazazi wao kwa magonjwa masuala kama hayo, ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimesisitiza kwamba ni wajibu wetu sisi kama jamii kwa ujumla kuhakikisha kwamba watoto ambao wanatakiwa kwenda shule waende shule na kuna mpango wengine wanaweza kupelekwa VETA. Ni

jitihada za Serikali kuhakikisha kwamba watoto hawaishi katika mazingira magumu.

SPIKA: Mheshimiwa Fatuma Toufiq, Dodoma mnaambiwa watoto ni wengi, uliza swali.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa watoto hawa wadogo hawatumiki katika kubeba mizigo tu, lakini kuna wengine ambao hutumika kuwaongoza baadhi ya wazazi au walezi na watu wazima katika kwenda kuombaomba.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwanusuru watoto hawa?

SPIKA: Hivi mambo ya watoto, Wizara *specific* kabisa si ni Afya? Mbona mmekaa jamani? Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali, Mheshimiwa Ndugulile.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Toufiq kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara tumefanya sensa ya kubaini watoto ambao wanaishi mitaani au wanaoishi katika mazingira hatarishi katika baadhi ya Majiji na tumebaini idadi na wale ambao tuliwabaini na vyanzo vyao ambavyo vimewasababisha wao kuwa mitaani wengine tumeweza kuwaunganisha na wazazi wao, lakini vile vile, tunaendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba wale ambao tunawabaini hawana wazazi kabisa, tunawatunza katika nyumba zetu za kuwalelea watoto.

SPIKA: Mheshimiwa Bulembo nilikuona.

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na aliyejibu swali sasa hivi, Jiji ambalo lina watoto wengi kuliko hili, moja ya nane ya

Dodoma ni Jiji la Dar es Salaam. Hao wa Dar es Salaam ambao sasa limeitwa Jiji la Utalii, lina wageni wengi na ni wengi, yaani ni wengi kuliko; hatua zipi za makusudi zinachukuliwa kulifanya Jiji la Dar es Salaam kuondoa ombaomba ili hawa watalii wanaonyang'anywa, wanaoibiwa waweze kuwa na raha katika Jiji la Dar es Salaam? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Bulembo anasema Jiji lenye watoto wanaozurura wengi sana ni Dar es Salaam, lakini mimi nadhani Jiji linaloongoza kwa watoto wengi wanaozurura ni Mwanza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali. Mheshimiwa Naibu Waziri labda utatupa na takwimu, Jiji lipi linaongoza kwa watoto wazururaji? Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, sina takwimu za papo kwa papo, lakini kwa ujumla najua katika sensa yetu tuliyoifanya, tulibaini kama watoto zaidi 6,000, lakini nahitaji nifanye uhakiki kujua katika Majiji haya ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Arusha, Dodoma na maeneo mengine ni wapi ambapo takwimu zipo nyingi.

Mheshimiwa Spika, nimwahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hiyo taarifa tutampatia. Sisi kama Wizara, tumeendelea kulifanyia kazi suala hili, lakini kama alivyosema katika jibu la msingi la Mheshimiwa Kandege ni kwamba jukumu la malezi ya mtoto ni la familia. Pale inaposhindikana ni jamii ambayo inaizunguka na mwisho pale inapoonekana kabisa hakuna wa kuwasaidia wale watoto, sisi kama Serikali tunachukua majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kutoa rai kwa jamii kuhakikisha kwamba tunatimiza majukumu yetu ya msingi ya kuwalea watoto kama ilivyoainishwa katika sheria.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hebu fanyeni uamuzi katika hili. Jiji linaloongoza kwa watoto wengi wanaozurura, maana ninyi mnatembea sehemu nyingi? Ni Jiji gani?

WABUNGE FULANI: Dodoma.

SPIKA: Mwanza imeshinda. (*Kicheko*)

Wizara ya Nishati Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, uliza swali lako tafadhali.

Na. 11

Tatizo la kukatika kwa Umeme Kigamboni

MHE. LUCY S. MAGERELI aliuliza:-

Wilaya ya Kigamboni inakabiliwa na tatizo la msongo mdogo wa umeme na matukio ya kukatika umeme ya mara kwa mara hata mara tatu kwa siku:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukomesha tatizo hilo?

SPIKA: Majibu la swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Subira Mgalu, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na tatizo la umeme kupungua nguvu (*low voltage*) katika maeneo ya Manispaa ya Mji wa Kigamboni kutokana na uchakavu wa mifumo ya umeme pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya umeme kutokana na kasi ya ujenzi wa nyumba za makazi na viwanda. Serikali kupitia *TANESCO* inaendelea na kazi ya kuboresha hali ya umeme (*voltage improvement*) kwa

kuongeza njia za umeme na *transformer* katika maeneo ya Kigamboni yakiwemo Vijibweni, Kibugumo, Kibada, Uvumba, Kisota, Maweni na Kwa Thoma.

Katika kushughulikia tatizo hili, Serikali kupitia *TANESCO* mwaka 2017 ilifanya matengenezo kwa ajili ya kuboresha Kituo cha Kupooza Umeme Kigamboni kwa kukiongezea uwezo wake kutoka *MVA 5* iliyokuwa inahudumia wateja 3000 kufikia *MVA 15* yenye uwezo wa kuhudumia wateja 12,000. gharama ya mradi ni shilingi 1,500,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha ujenzi wa Kituo Kipya cha Kupooza Umeme cha Kurasini cha 132/33KV kitakachopeleka umeme wa uhakika katika maeneo ya Kigamboni. Ujenzi wa kituo hicho ulianza mwaka 2018 na utakamilika mapema mwezi Aprili, 2019 na hivyo kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine Serikali kupitia *TANESCO* inaendelea na kazi ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 kutoka Kurasini hadi Dege na ujenzi wa kituo kipya cha kupoza umeme cha *MVA 120* katika eneo la Dege Kigamboni. Mradi huu ulianza kutekelezwa kuanzia mwezi Januari, 2018 kwa gharama ya shilingi bilioni 16 na utakamilika ifikapo Septemba, 2019. Kukamilika kwa mradi huu kutaimarisha na kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme katika maeneo ya Mbagala na Kigamboni na hivyo kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo la kukatika umeme kwa Wilaya za Kigamboni na Temeke. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Magereli nimekuona, tafadhali uliza swali la nyongeza.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri mwenyewe kwamba tatizo hili lipo Kigamboni na ni kubwa. Katika majibu yake unaona anaeleza kabisa kwamba umeme

unaopatikana Kigamboni unakidhi kuhudumia wateja 12,000 tu, wakati wakazi wa Kigamboni ni zaidi ya 300,000.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikifuatilia suala hili tangu mwaka 2016 Mheshimiwa Muhongo akiwa Waziri wa Nishati, majibu ni haya haya. Mheshimiwa Mgalu yeye ni shahidi, nimeshakutana naye mara kadhaa tukijadiliana suala hili hili na majibu yamekuwa ni haya haya. Je Serikali ina nia thabiti ya kuondoa tatizo hili Kigamboni kweli?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika majibu yake Mheshimiwa Waziri ameonesha kwamba kuna ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kurasini cha KVA 132, ambacho anaeleza kwamba kinakamilika mapema Aprili, 2019. Tunavyozungumza leo ni mapema Aprili, 2019, je, kituo hiki kimekwishakamilika?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Subira Mgalu, tafadhali.

NAIBU WAZIRI NISHATI: Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza la nyongeza, Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba majibu ni yale yale na nini mkakati wa Serikali. Nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge majibu si yale yale kwa sababu zipo hatua zinazoendelea na tatizo la kukatikakatika kwa umeme hususan siyo Kigamboni tu katika Jiji la Dar es Salaam, ni kutokana na kuongezeka kwa mahitaji na kuzidiwa kwa kituo cha Ubungo cha jumla. Nini Serikali imefanya; yapo matengenezo makubwa pia yanaendelea pale Ubunge ambapo kwa sasa kituo kile ambacho kilikuwa na uwezo wa kusafirisha umeme wa megawati 635 kwa ujumla kwa Mkoa wa Dar es Salaam na mahitaji yake ni megawati 500 lakini inapotokea kwa mfano kituo cha *Songas*, kituo cha Tegeta, kinapotokea matengenezo ya mtambo mojawapo lazima kunakuwa na upungufu wa umeme katika maeneo mbalimbali ikiwepo Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwenye jibu langu la msingi nimesema kwamba hatua zilizochukuliwa zaidi ya bilioni 16 zimewekezwa katika kituo cha Dege; zaidi ya bilioni

1.5 zishatumika. Kwa hiyo, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge nia ya dhati ipo na si kwa Kigamboni tu, bali kwa maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dar es Salaam na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge dada Lucy anaulizia kwamba ujenzi wa hiki kituo ambacho nimekitaja Dege nimesema mapema Aprili, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo hiki mpaka ifikapo tarehe 30 mwezi wa Aprili kitakuwa kimeanza kufanya kazi. Pia alisema kwamba umeme katika kituo cha Kigamboni kinahudumia watu 12,000, nataka nimtaarifu kituo cha Mbagala pia kinahudumia wakazi wa Kigamboni na umeme mwingine ambao unatokea Ubungo. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuona Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira, uliza swali lako.

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba niulize swali dogo la nyongeza; kwa kuwa matatizo ya Wilaya ya Kigamboni yanafanana kabisa na matatizo ya Wilaya ya Mvomero; kwa kuwa katika Wilaya ya Mvomero, Kata ya Kibati kuna tatizo kubwa sana la msongo wa umeme na hivi ninapozungumza leo hapa Bungeni hakuna umeme Kibati kutokana na transfoma ya Kibati kuungua kwa zaidi ya mwezi mmoja sasa na wananchi wa Kibati wako gizani.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kufanya ziara na mimi Kibati ili kuondoa tatizo hili ambalo wananchi wanateseka?

SPIKA: Kwa ruhusa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Spika ndiyo itawezekana hiyo ziara. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Murad Saddiq, Mbunge wa Mvomero kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tumepokea hiyo changamoto ambayo anasema katika Kata ya Kibati transfoma imeharibika, si tu kwamba inahitaji nifanye ziara bali inatakiwa wananchi hawa wapate huduma haraka, kwa hiyo naiagiza *TANESCO* Mkoa wa Morogoro suala la kuharibika kwa *transformer* halisubiri ziara, inatakiwa wafanye matengenezo haraka iwezekanavyo ili huduma iendelee.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nataka nilisemie kwa ujumla; nimesema kwamba kuna matengenezo makubwa yanafanyika Mkoa wa Dar es Salaam kituo cha Ubungo ambacho kinapokea umeme kutoka Kidatu kwa njia ya msongo kilovoti 220 ambao unafika Morogoro unapoozwa unapelekwa Dar es Salaam. Kwa hiyo, matengenezo ya Dar es Salaam kwa kweli yana athari za moja kwa moja na upungufu wa Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Tanga; nichukue fursa hii kuwapa pole wakazi wa mikoa hii na kuwaomba radhi, lakini tuvumilie mwezi Aprili, mwaka huu 2019 yakikamilika matengenezo yale makubwa ambapo yamegharimu zaidi ya bilioni 32 hali itatulia.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Joseph Mkundi, Ukerewe huko hali ikoje?

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Tatizo la kukatika kwa umeme limekuwa linajitokeza sana kwenye Visiwa vya Ukerewe hali inayoathiri shughuli za kiuchumi na hasa shughuli za utoaji wa huduma za afya kwenye hospitali yetu ya Wilaya ya Nansio.

Ningependa kupata kauli ya Serikali, ni mkakati gani uliopo kuondoa tatizo hili na kufanya Visiwa vya Ukerewe vipate umeme bila shida ya kukatikatika kwa umeme kwenye maeneo hayo. Nashukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Visiwani huko Ukerewe (UK), umeme shida, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkundi Mbunge wa Ukerewe kupitia Chama cha Mapinduzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Mbunge aliwasilisha hilo leo asubuhi kwamba kuna tatizo hilo katika Visiwa vya Ukerewe na hapa nilipo nishatoa maelekezo kwamba kwa sababu umeme wa Ukerewe unatokea katika maeneo ya Bunda na kwa changamoto ambayo nimeipata hivi asubuhi baada ya kuwasiliana na Meneja kwamba kuna tatizo la changamoto ya nguzo, ndiyo maana Serikali imefanya maamuzi ya kuhama sasa itumie nguzo za zege.

Kwa hiyo, tumetoa maelekezo ifanyike utafiti wa kina changamoto ni nini ili ifanyiwe kazi, kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Mbunge baada ya kutoka hapa tufanye mazungumzo ili kuweza kumpa mikakati ambayo Serikali imepanga. Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Tuendeleo Waheshimiwa, bado tuko Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Mbunge wa Kibiti, Mheshimiwa Ally Seif Ungando, tafadhali uliza swali lako, kwa niaba yake Mheshimiwa Vullu.

Na. 12

Kupeleka Umeme kwenye Kituo cha Afya Mbwera Kibiti

MHE. ZAYNABU M. VULLU (Kn.y. MHE. ALLY S. UNGANDO) aliuliza:-

Ukarabati wa Kituo cha Afya Mbwera yakiwemo majengo ya upasuaji, Wodi ya Wazazi na mengineyo unakwenda kwa kasi sana:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka umeme kwenye Kituo cha Afya Mbwera?

(b) Je, ni lini kazi hiyo itaanza?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Mgalu tafadhali, Naibu Waziri wa Nishati.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali itapeleka umeme katika Vijiji vya Mbuchi, Mbwera Mashariki na Mbwera Magharibi kupitia utekelezaji wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini (REA) III unaoendelea. Kazi hiyo itaanza Mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2021. Mradi huo unahusisha kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa katika eneo la Mbwera kutoka Muhoro kwa kujenga njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 40; ujenzi wa njia ya kusambaza umeme yenye urefu wa kilomira 2.78; ufungaji wa transfoma moja (1) ya KVA 50; pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 48 ikiwemo Kituo cha Afya cha Mbwera. Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 1.56. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Zaynabu Vullu, swali la nyongeza, tafadhali.

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mbunge wa Jimbo la Kibiti Mheshimiwa Ally Seif Ungando na wananchi wa Kibiti, napenda kuipongeza na kuishukuru Serikali kwa juhudi ilizofanya, lakini pamoja na hayo, nina maswali mawili. Kwa kuwa umeme umeshafikia hatua hiyo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri amielezea, ningependa kujua ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye maeneo ya Nyatanga, Kingwira, Zimbwini, Runyozi na Makaoni?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali iliahidi kaya 90 katika eneo la Kitembo na katika kaya hizo 90, kaya 40 bado hazijapata umeme, ningependa kujua Serikali imejipangaje katika hilo? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Zainab Vullu, Mbunge mwenzangu wa Viti Maalum wa Mkoa wa Pwani.

Katika maswali yake mawili ya nyongeza, amepongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge Ally Seif Ungando na mimi nimepokea kwa niaba ya Wizara, kwa kazi ambayo inaendelea katika maeneo ya Wilaya ya Kibiti na katika maeneo mbalimbali, lakini ameulizia maeneo ya Nyatanga, Zimbwini, yatapata lini umeme. Nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge mama Vullu kwamba katika *REA III* mzunguko wa pili unaoendelea, maeneo haya yameingizwa katika orodha na kazi inatarajiwa kuanza 2019 mwezi wa Saba. Nalitarajia Bunge hili wakati wa kuwasilisha Bajeti yetu ituunge mkono ili kazi ya kumaliza vijiji ambavyo vimesalia katika mradi wa *REA III* mzunguko wa kwanza viweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ameelezea eneo la Kitembo nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na kumshukuru kwa sababu ni moja ya maeneo ambayo tunayatembelea kwenye ziara mimi pamoja na yeye Kitembo tumewasha umeme kama anavyosema, tumeshawaunganisha kaya 50, hizi kaya 40 kwa sababu mradi unakuwa na wigo wa wateja wa awali. Mradi unakuwa na kazi za awali, kaya zinazobaki *TANESCO* inaendelea na kazi yake ya kusambaza umeme. Kwa hiyo, naomba nielekeze *TANESCO* kuzingatia kwamba mradi unapokamilika na kukabidhiwa waendeleo kuwasambazia umeme wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inaongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli imefanya uamuzi wa kiseru, kwamba kwa sasa umeme utakaosambazwa na *TANESCO*, *REA* na wadau wowote, bei ya kuunganisha ni shilingi 27,000/=. Kwa hiyo hakuna kikwazo kingine kwamba kutakuwa na bei nyingine pengine shilingi 177,000/=, bei ni

moja shilingi 27,000/=; kwa hiyo *TANESCO* waendelee na kazi ya kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali ambao mradi wa *REA* umekamilika. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Subira jaribu kuangalia tu jinsi ambavyo matatizo ya umeme yalivyo makubwa. Kwa hiyo, iko haja Wizara ya Nishati kuona tu hali. Nilikuona Mheshimiwa Edwin Sanda, swali la nyongeza, tafadhali.

MHE. EDWIN M. SANND: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwenye Kata ya Kolo, Jimbo la Kondoa Mjini tulipata ufadhili mkubwa sana wa wenzetu wa MKAJI kwa ajili ya kukarabati Zahanati kwa lengo la afya ya mama na mtoto, na waliweka lengo kubwa sana mkazo mkubwa kwenye huduma ya maji, kimekarabatiwa kisima kirefu, kimemalizika sasa hivi takriban miezi mitatu. Kinachokwamisha ni *supply* ya umeme pale ili huduma hiyo iweze kuanza kutumika. Tumewaomba *TANESCO* Wilaya, *TANESCO* Mkoa mpaka sasa hivi bado tunasubiria. Je, ni lini sasa wenzetu wa *TANESCO* watatuletea ule umeme ili zoezi zima la wenzetu wa MKAJI lianze kuleta tija?

SPIKA: Swali hilo ni *very specific*, la mahali pamoja peke yake, sijui kama Mheshimiwa Naibu Waziri utalijaribu, tafadhali kama una la kusema.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sannda, Mbunge wa Kondoa Mjini, kwamba hili swali lake ni zuri linahitaji utekelezaji, nimwahidi Mheshimiwa Mbunge baada ya kipindi cha maswali na majibu na ratiba ya Bunge tukutane na pia nitafanya ziara maalum na wataalam wa *TANESCO* katika maeneo hayo ili kuhakikisha kisima hiki kinapata huduma hii ili dhamira iliyotarajiwa kwa ujenzi wa zahanati na ukarabati hiyo iweze kufikiwa, ili iweze kupata maji na huduma iweze kutolewa. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Sasa tuendelee na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kuna maswali mawili pale. Swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Galloss.

Na. 13

Raia wa Kigeni Wanaozalisha Ndugu zetu na Kuondoka

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani juu ya raia wa kigeni wanaopewa vibali vya kuja kufanya kazi hapa nchini kwa muda na kuwazalisha watoto na wadogo zetu na inapofika muda wa kuondoka huwakimbia na kuwaacha watoto hao wakiishi maisha yao yote bila baba kitu ambacho huwasababishia unyonge katika maisha yao?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamad Masauni, *Engineer*.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Magharibi, kama lfuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Idara ya Uhamiaji inatoa vibali vya ukaazi nchi kwa wageni baada ya Wizara ya Kazi kutoa vibali vya kazi kwa wageni hao.

Mheshimiwa Spika, mikakati ambayo Serikali inachukua ni kuelimisha raia wa Tanzania kuwa wasidhani kila mgeni anayekuja kufanya kazi Tanzania ni mtu mwema au ana uwezo wa kifedha na kutegemea kuwa atasaidiwa na mtoto wake kwenye malezi, hivyo kuwa waangalifu ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea kutokana na kujiingiza kwao katika mahusiano ya kimapenzi na watu

wasiowafahamu vema ikiwemo mimba na maradhi yanayosababishwa na ngono.

SPIKA: Mheshimiwa Tauhida, nimekuona swali la nyongeza tafadhali.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuuliza maswali mawili. Ningependa kufahamu njia gani zinazotumika katika kutoa elimu hiyo hususan vijijini?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili kwa kuwa Mkuu wa Mkoa amekuwa mdau mkubwa wa kuwapigania watoto wanaoachwa na wazazi wao wa kiume, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuja na sheria za kuwabana wanaoacha watoto hususan wakiwemo na raia wa kigeni.

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Kange Lugola, tafadhali.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Tauhida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa tunayo sheria ambayo inaharamisha matukio ambayo yanahusisha mtu yeyote kutelekeza mtoto ama kutotoa matunzo na sheria hiyo si nyingine ni Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 kifungu cha 166, kwa hiyo sheria tunayo tayari. Niwaombe akinamama wote ambao wameathirika na jambo hili kwa kuwa ni la jinai, waende kwenye vituo vya polisi vilivyo karibu wafungue kesi hizi ili Serikali tutumie sheria nyingine zozote tulizonazo za kuwarejesha nchini wajibu mashtaka.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo zoezi alilolifanya Mheshimiwa Makonda Mkuu wa Mkoa ambalo Mheshimiwa Mbunge ame-*refer* ni zoezi ambalo lilionyesha dhahiri kwamba sio wageni tu wanaotelekeza watoto isipokuwa

hata Watanzania wanatelekeza watoto na tulishuhudia wengine humu ndani sura za watoto zikiwa zinawafanana.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa akinamama wa Tanzania, nawaomba mtumie kilicho ndani ya nchi, kilicho chenu kuliko kuanza kukimbilia kutumia raia wa kigeni ilhali hata humu ndani, rudini humu ndani kumenoga.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Nakubaliana na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kabisa asilimia mia moja na mimi nishuhudie ninayo mawasiliano kadhaa ya akinamama kutoka sehemu mbalimbali za nchi yetu wakiwalalamikia Wabunge wanaume kutelekeza watoto. Sasa naomba kila anayehusika na jambo hilo achukue hatua, iko siku hapa nitakuja na orodha, itakuwa tabu tena, patakuwa hapatoshi. *(Kicheko)*

Bado tuko Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Victor Kilasili Mwambalasa, Mbunge wa Lupa.

Na. 14

Hitaji la Gereza Chunya

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Gereza katika Wilaya ya Chunya.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalasa, Mbunge wa Lupa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi sasa nchini kuna Wilaya 51 ambazo hazina Magereza ya Wilaya ikiwemo ya Chunya. Hata hivyo, lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa kila Wilaya

inakuwa na Gereza ili kuwahifadhi wahalifu wa Wilaya husika, kwani uwepo wa Gereza kwenye kila Wilaya utapunguza gharama za kuwasafirisha wahalifu kutoka Wilaya moja na kuharakisha uendeshwaji kesi sambamba na kupunguza msongamano wa mahabusu.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali inaendelea na mpango wa ujenzi wa magereza kwa awamu kwenye Wilaya zisizokuwa na magereza. Hata hivyo, kasi ya ujenzi huo imekuwa ni ndogo kutokana na kuathiriwa na uhaba wa rasilimali fedha. Hivyo Serikali inadhamiria kujenga na kuendelea na ujenzi huo kwenye Wilaya zisizo na Magereza ikiwemo Wilaya ya Chunya kadri ya hali ya Bajeti itakavyoruhusu.

SPIKA: Mheshimiwa Mwambalasa, swali la nyongeza.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Serikali imetoa majibu kitaalam sana na Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri mwenyewe kwamba uwepo wa gereza mahall unapunguza gharama za usafiri, unaharakisha uendeshaji wa kesi, vilevile unapunguza msongamano magerezani ambao ni kubwa sana kwa sasa. Pamoja na majibu hayo mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Chunya ni Wilaya kongwe sana hapa nchini. Katika Wilaya tatu kongwe Chunya imo, mwaka huu inatimiza karibu miaka 80. Je, rasilimali fedha itakapopatikana Mheshimiwa Waziri ananihakikishia kwamba ataipa Chunya kipaumbele kujenga gereza Wilayani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika kipindi cha mpito kabla ya kujengwa kwa gereza hilo, je, Serikali ipo tayari kujenga walau chumba, siyo gereza, chumba cha mahabusu ili kuweza kupunguza gharama hizi ambazo Serikali imezisema? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Eng. Hamad Yussuf Masauni, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Victor Mwambalasa, Mbunge wa Rukwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pale bajeti itakapokaa vizuri Chunya itakuwa eneo la kipaumbele. Kwanza, nichukue fursa hii kumpongeza yeye binafsi kwa kushirikiana na wananchi wa eneo hilo kuanza mchakato ambao unaendelea wa ujenzi wa bweni moja na jengo la kuishi Askari ambao umefikia 90%.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yetu kwamba litakapokamilika kwa 100% tutaanza kupeleka wafungwa na kuanzisha kambi ambapo wafungwa hao tutawatumia kwa ajili ya kufyetua matofali ikiwa ni maandalizi ya ujenzi wa gereza. Wakati tunasubiri bajeti ikae vizuri Serikali tutaunga mkono nguvu hizo kwa kuhamasisha wafungwa na kutumia rasilimali zilizopo Chunya ili tuweze kutatua tatizo hili angalau kwa kuanzia gereza la mahabusu ili kupunguza msongamano.

SPIKA: Swali la nyongeza, Mheshimiwa John Mnyika nilikuona uliza swali fupi.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri amesema ujenzi wa magereza katika maeneo mbalimbali vilevile utasaidia kupunguza msongamano wa mahabusu. Pia amesema kuwa ujenzi huo kwa sasa unakwamishwa na uhaba wa rasilimali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ujenzi huu hauwezi kuendelea kwa haraka kwa sasa; na kwa kuwa kuna msongamo mkubwa wa mahabusu katika magereza mbalimbali kutokana na kubambikiziwa kesi ama mashtaka yasiyokuwa na dhamana na hukumu ambazo kimsingi zinajaza tu magereza yetu, je, Serikali ipo tayari sasa

kutekeleza operesheni maalum ya kupunguza mahabusu katika magereza mbalimbali nchini? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, tafadhali Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nirekebishe kauli yake si kwamba msongamano wa mahabusu chanzo chake kikubwa ni ubambikiziwaji wa kesi. Tunajua tuna changamoto ya ubambikiziwaji wa kesi na pale ambapo tunabaini na tumekuwa tukifanya kazi hiyo ya kuhakikisha wale ambao wanahusika na upambikaji kesi wanachukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, lakini msongamano wa mahabusu unatokana na changamoto za uhaba wa magereza. Magereza yetu yamejengwa muda mrefu na idadi ya watu inaongezeka na changamoto ya uhalifu inasababisha msongamano huu pia kuongezeka. Hata hivyo, Serikali tumefanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha kwamba tunapunguza msongamano huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake kuhusu operesheni, hivi tunavyozungumza tuna utaratibu wa kamati za kuharakisha kesi ambazo zinahusisha wadau mbalimbali ambapo wanahakikisha wale ambao wanatakiwa dhamana kwa haraka wanasikilizwa. Vilevile, tumekuwa tukitumia sheria zetu mbalimbali, kwa mfano, Sheria ya Bodi ya *Parole*, Sheria ya Huduma za Jamii, Sheria ya *EML* na msamaha Mheshimiwa Rais ambao amekuwa akitoa kila mwaka, yote haya yanasaidia kupunguza msongamano wakati Serikali ikiendelea na jitihada zake za kujenga mabweni na kuongeza na kupanua idadi ya magereza yetu ili yaweze kuchukua idadi kubwa zaidi ya wafungwa.

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimpe nafasi Mheshimiwa Naibu Katibu Mkuu wa *CUF* mpya Mheshimiwa Magdalena Sakaya. *(Makofi)*

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014 Serikali ilitenga eneo la hekari zaidi ya 30 katika Kata ya Ushokora kwa ajili ya kujenga Gereza la Wilaya lakini kwa miaka sita (6) sasa wananchi wa Pozamoyo pale Ushokora hawajawahi kuambiwa chochote na waliondolewa kwenye makazi na mashamba yao wameenda kujibanza kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani sasa angalau kufidia wananchi wale iliyowahamisha pale ambao wamepanga maeneo mbalimbali waweze kwenda kutafuta makazi sahihi na wakati huo huo Serikali iweze kujenga hilo gereza maana ni muda mrefu sasa? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Kaliuwa na Naibu Katibu Mkuu mpya wa Chama cha *CUF*, kama ifuatavyo:- *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nimeelewa vizuri swali lake anazungumzia wananchi ambao wametakiwa kuhamishwa kwa ajili ya ujenzi wa gereza na ambao pengine anadhani wanahitaji kulipwa fidia. Kama hivyo ndivyo kwa sababu swali lake hili ni mahsusi naomba nilipokee na tuweze kulifanyia kazi na nitampatia mrejesho.

SPIKA: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kama ilivyo kwa Wilaya ya Chunya, Wilaya ya Kyela haina mahabusu ya wanawake hivyo kupelekea kupelekwa Wilaya ya Rungwe. Je, ni lini Serikali itajenga mahabusu ndogo ya wanawake kwa Wilaya ya Kyela?

SPIKA: Majibu mafupi kwa swali hilo, lini mnajenga kule Kyela gereza la akina mama?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimezungumza kwamba changamoto inayosababisha tusiwe na ujenzi wa magereza yetu ambao siyo wa kasi kubwa sana ni kutokana na ufinyu wa bajeti. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Gereza la Wanawake Kyela ni miongoni mwa maeneo ambayo tunayaangalia kwa jicho la kipaumbele sana. Kwa hiyo, pale ambapo bajeti itakaa vizuri Gereza la Wanawake Kyela litakuwa ni jambo la kipaumbele.

SPIKA: Tunahamia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swali linaulizwa na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga.

Na. 15

Kukithiri kwa Masuala ya Ubakaji na Mapenzi ya Jinsia Moja nchini

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA aliuliza:-

Masuala ya kunajisi na ubakaji kwa watoto pamoja na mapenzi ya jinsia moja yamekithiri nchini na kuongezeka siku hadi siku:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya utafiti wa kina na kuona athari zinazoendelea kuikumba jamii katika suala zima la usagaji (*lesbianism*)?

(b) Je, ni lini Serikali itaanza kuandaa sheria ya kuwaadhibu wanawake wanaoharibu vijana wa kiume chini

ya umri wa miaka 18 na wale wenye kuwafunza na kuwaharibu watoto wetu wa kike katika masuala ya usagaji (*lesbianism*)?

SPIKA: Naibu Waziri Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndungulile, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 inakataza vitendo vilivyo kinyume na maadili ikiwemo mapenzi ya jinsia moja. Hadi sasa Serikali haina takwimu za hali ya usagaji na ushoga nchini. Hivyo, Serikali inaona umuhimu wa kufanya utafiti wa kina kuhusu masuala ya mapenzi ya jinsia moja ikiwepo usagaji ili kubaini ukubwa na athari za suala hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, pindi utafiti utakapofanyika, Serikali itaangalia uwezekano wa kuzifanyia marekebisho na kuboresha sheria zilizopo ili kubaini na suala hilo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Serikali inatambua kuwa sheria pekee haitoshi kutatua tatizo hili, hivyo inaendelea kutoa elimu kuhusu malezi chanya yanayozingatia maadali ya Kitanzania.

SPIKA: Mheshimiwa Najma nimekuona, swali la nyongeza.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nashukuru Serikali kwa kukubali na kuelewa kwamba suala hili linatambulika na lipo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijauliza maswali yangu mawili ya nyongeza, nataka ieleweke kwamba suala hili kama ilivyo ushoga yaani *Lesbianism* ni masuala ya usiri sana, kwa hiyo, kuyajua kwake siyo rahisi sana. Kwa hiyo, kwanza ningepomba Serikali isicheleweshe jambo hili la utafiti ili tuweze kujua kiwango cha athari hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nataka ieleweke na itambulike kwamba kunyamaza kwetu kimya sasa hivi na kuogopa mambo haya miaka 50 ijayo ndani ya Bunge hili badala ya kujadili maandeleo na maadili mema ya Kitanzania watakuja kujadili namna gani ya kupitisha ndoa ya jinsia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa narudi kwenye maswali yangu ya nyongeza. Swali la kwanza, nashukuru Serikali imeona umuhimu wa kutoa elimu pamoja na kwamba kuna sheria ambazo zinadhhibiti suala hilo na baada ya utafiti wamesema pia watafanya marekebisho ya sheria. Swali langu lipo hapa, je, wakati tunaendelea kufanya utafiti huo, kwa nini sasa Serikali isishirikiane Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya kuona namna gani bora wanaweka mitaala katika shule zetu na kuonyesha madhara na athari ya mambo haya ambayo ni kinyume cha maadili ya Tanzania ili wanafunzi wetu ambao wanasoma waanze kujengeka na misingi ya maadali na kuachana na mambo haya popote watakapoyaona? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ni kwamba tuna wanazuoni wengi sana katika Taifa hili wa dini mbalimbali, kwa nini Serikali sasa hakai nao na ikawataka watoe mahubiri ya kukataza masuala hayo ambayo Mwenyezi Mungu ameyakataza badala ya mambo mengine ambapo haya hawajayatilia mkazo? Maswali yangu ni hayo. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Ndungulile majibu kwa swali hili muhimu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu

maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Najma Giga ambaye ameongea kwa uchungu sana.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ameuliza kwa nini Wizara ya Afya isikae pamoja na Wizara ya Elimu kuangalia mitaala ili masuala haya ya maadili yaweze kufundishwa katika shule mbalimballi. Tunapokea ushauri wake na sisi kama Serikali tutaenda kuufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ameuliza kwa nini tusiwatake wanazuoni nao wakatoa mahubiri kuhusiana na suala hili. Moja ya taasisi ambayo imekuwa inatujenga katika maadili mema ni pamoja na taasisi zetu za kidini. Kwa hiyo, naamini nao wanatusikiliza kupitia Bunge lako hili Tukufu na wao tuwaombe wachukue majukumu yao ya msingi kuhakikisha kwamba wanahubiri maadili mema ya kitaifa vilevile wanawajenga waumini wao katika maadili mema yanayozingatia misingi yetu ya maadili ya kitaifa. Kwa hiyo, sisi kama Serikali hatuwezi kusema taasisi za dini zifanye lakini taasisi za kidini nazo zina wajibu kuhakikisha kwamba zinajenga waumini wao na Watanzania katika msingi ya maadili mema.

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kuna jambo moja ni vizuri nikawaeleza, liliulizwa swali la watoto Dodoma hapa limeendelea kuwa linasumbua lakini niwataarifu mnaoenda sokoni au maeneo ya standi na kadhalika ukimbebesha mtoto yeyote yule mzigo katika watoto wale tuliokuwa tunazungumza wazururaji ukikamatwa unalipishwa Sh.50,000 hapo hapo. Kwa hiyo, naomba mlifahamu hilo na hivyo tusiendekeze jambo hili la kuwabebesha mizigo watoto ili waweze kwenda shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ally Saleh nilikuona, uliza swali lako la nyongeza.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Tatizo la ubakaji watoto linaoneka ni

kubwa sana Mkoani Mara. Kamati ya Katiba na Sheria juzi ilikwenda Mara na tukapata taarifa za kutisha kutoka kwa Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Malima. Kuna Mwalimu kwa mfano amewafanya wake zake watoto 10 wa darasa la kwanza.

MBUNGE FULANI: Darasa la kwanza?

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Spika, nitarudia, amewafanya wake zake watoto 10 wa darasa la kwanza.

MBUNGE FULANI: Aaaaah.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Spika, kuna taarifa nyingi za kutisha juu za ubakaji kwa rika zote, kwa watu wazima na kwa watoto. Je, Serikali ama kupitia Wizara ya Afya au Bunge haioni haja sasa ya kuunda Tume au ya kutafuta utaratibu wa kwenda kulitazama tatizo hili ambalo ni kubwa inafika watu wanauliwa? Risasi zinatumika halafu watu wanakimbia upande wa pili wa Kenya inakuwa vigumu kulishughulikia. Mkuu wa Mkoa Adam Malima alikuwa na *pain* kubwa alipokuwa akituelezea juu ya suala hili. Naomba Serikali ifikirie jambo hili, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko, kumbe mnaongoza siyo tu kwa mambo mengine na hayo pia? Waziri wa Habari, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, tafadhali majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, pamoja na shinikizo kubwa kutoka nchi za Magharibi, shinikizo la ndoa za jinsia moja, shinikizo la kuuona ushoga kama haki za binadamu, bado nchi 38 kati ya nchi 54 za Afrika zinapinga masuala hayo na Tanzania ni mojawapo. Si hivyo tu, sisi tume-*criminalize* yaani vitendo hivyo ni makosa ya jinai na watu wanafungwa. Kwa hiyo, bado sisi ni moja ya nchi ambazo tumekaa vizuri katika kulinda jamii yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ni kwamba jamii inaficha haya matatizo. Kwa mfano, matatizo ya watoto

kulawitiwa au kubakwa kwa sehemu kubwa yanafanywa na ndugu katika jamii. Tukianza upelelezi familia zinawalinda hawa watu hawatoi ushahidi, ni tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika sheria kama hakuna ushahidi huwezi ukamfunga mtu na kosa hili ni kubwa, adhabu ni kali sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe wito kwa Tanzania tatizo ni kubwa sasa, tunaomba ushirikiano kwa vyombo vya dola ili tuweze kuwapata hawa wahalifu wanaojaribu kuchafua *generation* ya kesho, kesho kutwa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo. Sisi hapa Bungeni mambo ya mapenzi ya jinsia moja bahati nzuri hakuna kabisa.

WABUNGE FULANI: Aaah. *(Kicheko)*

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba.

Na. 16

Mzunguko wa Fedha kuwa Mdogo

MHE. DAVID E. SILINDE aliuliza:-

Katika kipindi cha hivi karibuni wananchi wamekuwa wakilalamikia mzunguko wa fedha kuwa mdogo:-

Je, hali hiyo imesababishwa na nani?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania inatekeleza Sera ya Fedha inayolenga kusimamia mzunguko wa fedha unaoendelea na mahitaji halisi ya uchumi kwa lengo la kudumisha utulivu wa mfumuko wa bei na hivyo kuweka mazingira mazuri ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya mwaka 2017 kulitokea changamoto ya kuongezeka kwa mikopo chechefe ambayo kwa sehemu kubwa ilisababishwa na baadhi ya taasisi za fedha kutoa mikopo bila kuzingatia Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na Kanuni zake za mwaka 2008. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali ilichukua hatua ya kusimamia kwa karibu Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 pamoja na Kanuni zake ikiwa ni pamoja na kuhamisha fedha za taasisi za umma kutoka kwenye mabenki ya biashara kwenda Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hali hiyo, kuanzia Januari, 2017, Serikali kupitia Benki Kuu ilichukua hatua za kuongeza ukwasi kwenye uchumi ili kutatua changamoto ya kupungua kwa mzunguko wa fedha katika soko. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kushusha riba ya Benki Kuu (*discount rate*) kutoka asilimia 16 Machi, 2017 hadi asilimia 7 Agosti, 2018. Pili, Benki Kuu ilipunguza kiwango cha kisheria cha sehemu amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu na mabenki ya biashara (*Statutory Minimum Reserve Requirement, SMR*) kutoka asilimia 10 hadi asilimia 8 mwezi Aprili, 2017. Tatu, kuruhusu mabenki kutumia asilimia 10.0 ya sehemu ya *SMR* kama chanzo kimojawapo cha kusaidia hali ya ukwasi kwenye uchumi. Mwisho, Benki Kuu ilianzisha utaratibu wa kutoa mikopo ya muda maalumu kwa mabenki pamoja na kununua fedha za kigeni kutoka kwenye soko la jumla la mabenki ili kuongeza ukwasi kwenye uchumi.

Pili, Benki Kuu ilipunguza kiwango cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu na

Benki ya Biashara (*Statutory Minimum Reserve Requirement*) kutoka 10% hadi 8% mwezi Aprili, 2017.

Tatu, kuruhusu mabanki kutumia 10% ya sehemu ya *Statutory Minimum Reserve Requirement* kama chanzo kimojawapo cha kusaidia hali ya ukwasi katika uchumi.

Mwisho, Benki Kuu ilianzisha utaratibu wa kutoa mikopo ya muda maalum kwa mabanki pamoja na kununua fedha za kigeni kutoka kwenye soko la jumla la mabanki ili kuongeza ukwasi kwenye uchumi.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za Sera ya Fedha zimesaidia kuboresha hali ya ukwasi kwenye Benki za Biashara na kupunguza riba katika Soko la Fedha baina ya mabanki kutoka wastani wa asilimia 4.6 kwa mwaka unaoishia Februari, 2018 hadi asilimia 2.3 kwa mwaka unaoishia Februari, 2019. Kuongeza kwa mikopo ya sekta binafsi kutoka wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2017 hadi asilimia 7.3 Januari, 2019 na kupungua kwa riba ya mikopo kutoka wastani wa asilimia 21 mwaka 2016 hadi wastani wa asilimia 17 mwaka 2018.

Hivyo basi, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sasa hakuna tatizo la mzunguko mdogo wa fedha katika soko baada ya Serikali kuchukua hatua hizi. Pia mzunguko wa fedha katika uchumi unaendana na malengo na mahitaji halisi ya shughuli za kiuchumi zilizopo.

SPIKA: Mheshimiwa Silinde, swali la nyongeza.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, bado nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Benki Kuu ya mwezi Februari, 2019 kwa maana ya *Monthly Economic Review*, inaonyesha kwamba kasi ya ukuaji ya ujazo wa fedha imeshuka kutoka asilimia 7.5 mwaka 2018 mpaka asilimia 3.3 mwaka 2019.

Je, Serikali haioni kuwa utekelezaji wa Sera ya Fedha umeleta matokeo tofauti kwa ukuaji wa ujazo wa fedha kuanguka zaidi kuliko mwaka 2018? (*Makofi*)

Swali la pili; kasi ya ukuaji ya mzunguko wa fedha nchini ni moja ya kiashiria muhimu sana cha kasi ya ukuaji wa uchumi; na ushahidi unaonyesha kwa miaka 20 kwamba unapokuwa na kasi ya ukuaji wa uchumi ya 7% maana yake kasi ya mzunguko wa fedha unakuwa katika *double digit* kati ya asilimia 12 mpaka 15. Kwa kutumia kiashiria cha mzunguko wa fedha na mfumuko wa bei, kwa nini Serikali isiache kutoa taarifa za uongo humu ndani ya Bunge na kwa Umma kwamba uchumi unakua kwa 7% ilhali hali halisi ni chini ya 4%. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Naibu Waziri Fedha, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nianze na swali lake la pili kwa sababu ameisingizia Serikali, ni kwamba Serikali siku zote inasema ukweli na haijawahi kudanganya Bunge, wala kudanganya sehemu yoyote. Nayasema haya kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (*SADC*) uliomalizika wiki mbili zilizopita, Tanzania imepongezwa kwa ukuaji wa uchumi mzuri kwa mfululizo wa miaka mitano. Kwa hiyo, siyo kwamba Serikali inayasema haya ndani ya Bunge peke yake, hapana. Serikali inayasema haya ndani ya Bunge, nje ya Bunge na Shirika la Kimataifa la Fedha (*IMF*) kwa taarifa yake limeipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ukuaji mzuri wa uchumi kwa kuweka nyenzo nzuri zinazohakikisha ukuaji wa uchumi wetu kuwa imara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tusiwadanganye Watanzania, uchumi wa Tanzania uko imara. Kwa Afrika Mashariki sisi ni

wa kwanza na kwa Afrika sisi hilo ni jambo la kawaida. Nendeni kwenye *google*, *m-google* halafu mtajua nini tunachokisema. Uchumi wetu uko imara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uchumi wetu uko imara na tuna uhakika kama ambavyo *prediction* zetu zilionyeshwa. Kwa mwaka 2018 tutakua kwa asilimia 7.2 kama *prediction* zetu zilivyoonyesha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza, ni sahihi kabisa alichokisema kwamba ujazi wa fedha ukilinganisha mwaka 2018 na mwaka 2019 taarifa iliyotelewa na Benki Kuu, ujazi wa fedha umepungua. Hiyo haimaanishi kwamba uchumi haufanyi vizuri. Unaposoma ile taarifa, soma na sababu, kwa nini ujazi wa fedha umepungua?

Mheshimiwa Spika, ujazi wa fedha umepungua kwa sababu Watanzania sasa hata hapa ndani tukijaribu kuchukua simu ya kila mmoja wetu, ndani ya kila simu ya mmoja wetu kuna fedha za kutosha ndani ya simu yake na anafanya *transaction electronically* kwa siku zaidi ya jinsi ambavyo anafanya *cash transaction* kwa fedha taslimu halisi.

Kwa hiyo, kunapokuwa na ongezeko la *transaction electronically*, fedha halisi sokoni zinapungua, lakini fedha zilizopo kwenye mzunguko zipo za kutosha. Kama nilivyosema, sera yetu ya fedha inahakikisha mzunguko wetu wa fedha unalingana na shughuli za kiuchumi ambazo zinaendelea ndani ya Taifa letu. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Silinde, kama huna hela ni wewe tu bwana eeh! Sasa wewe, eeh! Wengine tuko vizuri.

Mheshimiwa Ritta Kabati, tafadhali. Kwa sababu ya muda Waheshimiwa, mkiangalia saa yetu, mtaona.

Na. 17

Madeni ya Wazabuni

MHE. RITTA E. KABATI aliuliza:-

Mheshimiwa Rais alitoa tamko kuwa Wazauni wote wanaoidai Serikali walipwe:-

Je, tokea tamko hilo litolewe ni Wazabuni wangapi wameshalipwa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo. Malipo ya Wakandarasi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Ernespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jumla ya wazabuni 2,048 wamelipwa madai yao tangu kutolewa kwa tamko na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 3 Januari, 2018 Ikulu, Jijini Dar es Salaam. Kati ya wazabuni 2,048 waliolipwa, wazabuni 1,277 walihudumia sekretarieti za mikoa na 771 walihudumia Wizara, Taasisi na Wakala za Serikali.

Aidha, jumla ya shilingi 199,064,014,966.64 zimetumika kulipa wazabuni hao, ambapo shilingi 3,729,605,175/= zimetumika kulipa wazabuni waliotoa huduma kwa sekretarieti za Mikoa na shilingi 195,334,409,791.64 zimetumika kulipa wazabuni wa Wizara, Taasisi na Wakala za Serikali. Aidha, madai haya yalilipwa baada ya uhakiki kufanyika.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu na wananchi wa Tanzania kwa ujumla kwamba, Serikali itaendelea kulipa madai mbalimbali ya wazabuni

kulingana na upatikanaji wa fedha sambamba na uhakiki wa madai husika. Aidha, ili kukamilisha zoezi la uhakiki kwa wakati, wazabuni wote wanaombwa kutoa ushirikiano hususan kuwasilisha taarifa na vielelezo sahihi vya madai yao pindi wanapotakiwa kufanya hivyo.

SPIKA: Mheshimiwa Ritta Kabati, tafadhali.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba niulize maswali madogo tu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba niipongeze Serikali kwa majibu yake mazuri, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa tamko lake ambalo limehakikisha kwamba wazabuni wote wanalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna baadhi ya wazabuni wakiwemo hata wa Mkoa wangu wa Iringa wameshafanyiwa uhakiki zaidi ya mara moja, lakini wanadaiwa na mabenki, wanadaiwa na TRA na wanatishiwa mpaka kuuziwa mali zao:-

Je, Serikali inawasaidiaje wasifilisiwe? Maana wengi wao tayari wameshapata maradhi na kufa na wengine wameshafilisika kabisa kwa ajili ya madeni ambayo wanadai Serikali. *(Makofi)*

Swali langu la pili; je, ni vigezo gani sasa vinatumika kwenye malipo ya madeni ya wazabuni hao? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza kuhusu msaada wa Serikali ili wananchi wetu wasifilisiwe, naomba kumwambia Mheshimiwa Rita na kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali yetu kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tunalipa madai pale yanapokuwa yamehakikiwa. Wananchi wetu

hawa wa Mkoa wa Iringa, kama wapo ambao madeni yao yamehakikiwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Ndani wa Serikali, basi tumekuwa tukiwasaidia mmoja baada ya mwingine wanapofika na kuwasilisha nyaraka zao kuonyesha kwamba wamehakikiwa na sisi kujiridhisha kwamba wapo kwenye orodha ya kulipwa ndani ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Ritta na nimpongeze kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya katika kuwatetea wananchi wa Iringa. Ameshakuja siyo mara moja wala mara mbili ofisini kwangu, naomba tuendelee kushirikiana ili tuwasaidie wananchi wetu ili wasifilisiwe na ili wasiendelee kupata maradhi kama wapo kweli waliopata maradhi. Tuendelee kushirikiana tuwasaidie wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, ameuliza ni vigezo gani vinavyotumika kulipa madai haya ya wazabuni pamoja na wakandarasi wengine? Kwanza kabisa ni kuhakikisha deni limehakikiwa na limekidhi vigezo vya kuwa deni halali. Hicho ni kigezo cha kwanza kwamba deni hilo linalipwa.

Mheshimiwa Spika, sababu ya pili au kigezo cha pili ambacho kinapelekea kulipwa, tunaangalia deni lile kama hali-*attract* riba kwa Serikali, lakini pia kwa yule ambaye anaidai Serikali. Kama deni hili lina-*attract* riba tunayapa kipaumbele ili Serikali isiendelee kuumia na ili tusiendelee kuwaumiza wananchi wetu ambao wanaidai Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, kigezo cha tatu ni kuhakikisha kwamba ukubwa wa deni lenyewe, kwa wale ambao wana madeni ambayo siyo makubwa na ambao ndio wengi tumekuwa tukiwapa kipaumbele kuhakikisha kwamba tunawalipa madeni yao kwanza ili kuweza kuchachua uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana mwaka 2017/2018 Bunge lako Tukufu lilitupitishia bajeti ya shilingi trilion moja kwa ajili ya kulipa madeni haya na Serikali ililipa zaidi ya shilingi

trilioni 1.096 kwa sababu dhamira ya Serikali yetu ni njema kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kigezo cha nne, ni umri wa deni. Madeni yale ambayo yamekaa kwa muda mrefu na tayari yamehakikiwa, tumekuwa tukiyapa kipaumbele na kuhakikisha yote yanalipwa ili kuwawezesha wananchi wetu kuendelea kushiriki katika shughuli za kiuchumi.

SPIKA: Ahsante sana. Swali la mwisho kwa siku ya leo linaelekezwa Maliasili na Utalii, litaulizwa na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze. Tafadhali.

Na. 18

Agizo la kutoondoa Vijiji vilivyomo maeneo ya Hifadhi

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE aliuliza:-

Katika kikao cha kazi, Mheshimiwa Rais akiwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dkt. Hamis Kigwangalla na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Abdallah Ulega alitoa maelekezo ya kutoondoa Vijiji vilivyomo katika maeneo ya Hifadhi:-

(a) Je, tangazo hilo linamaanisha kuwa wameruhusiwa kuendelea na shughuli za kiuchumi katika maeneo yao wanayoishi?

(b) Je, ni lini sasa Serikali itashughulikia migogoro ya mipaka baina ya Vijiji hivyo na Hifadhi au kwa tamko lile maana yake Wanavijiji waendeleo kama vile hakukuwahi kuwa na migogoro?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Januari, 2019, Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa agizo la kutoviondoa vijiji 366 vilivyoainishwa kuwa na migogoro na maeneo ya hifadhi. Aidha, alisisitiza kwamba agizo hilo halina maana kwamba sasa wananchi wanaruhusiwa kuvamia maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, baada ya Mheshimiwa Rais kutoa maelekezo hayo, Kamati Maalum kwa lengo la kumshauri Mheshimiwa Rais namna bora ya kutekeleza agizo hilo iliundwa. Kamati hii inaongozwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi. Wizara nyingine zinazohusika ni Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Wizara ya Maliasili na Utalii, Mifugo, Uvuvi, TAMISEMI, Ulinzi, Kilimo na Maji. Jukumu la Kamati litakapokamilika, taarifa itawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais na maelekezo yatatolewa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia Kamati kukamilisha kazi yake na taarifa kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais, Wizara ya Maliasili na Utalii itapitia upya mipaka ya hifadhi mbalimbali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati na maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Kazi hii itahusisha uwekaji wa vigingi vipya (*beacons*) katika mipaka yote.

SPIKA: Mheshimiwa Ridhiwani.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza na kumshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya, lakini pia kwa kutuliza joto la wananchi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na mambo mawili makubwa ambayo nilikuwa nataka niishauri Serikali. Kwanza,

nimwambie Mheshimiwa Waziri, sikusudii kumzungumza au kuwatetea wavamizi wa hifadhi hizo. Ila swali langu linalenga katika hifadhi zilizovamia vijiji vyetu, maana kesi ya watu wa Chalinze ni hifadhi imevamia vijiji.

Mheshimiwa Spika, la pili, nikushukuru na kukupongeza, naona leo umemwalika Bwana Pierre Liquid, ni jambo jema, lakini ushauri wangu naomba kwa Wizara, inapofanya kazi katika kuweka hivyo vigingi na *beacons* itushirikishe sana sisi wawakilishi wa wananchi ili tuweze kuwapa ushirikiano na kuwakumbusha vizuri ili wasije kuvuruga kabisa zoezi zima.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nipokee pongezi hizo ambazo amempa Mheshimiwa Rais. Ni kweli kwamba hata kabla ya tamko la Mheshimiwa Rais maeneo haya yamekuwa ndani ya migogoro mingine kwa zaidi ya miaka 20; na yapo maeneo ambayo yalikuwa yana *GN* mbili; eneo lina *GN* ya uhifadhi lakini pia kuna *GN* ya kijiji au kata katika eneo la hifadhi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais alichokifanya ni kulifanya tatizo hili liweze kushughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza, amesema kwamba hifadhi ndiyo zimevamia maeneo ya vijiji. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, baada ya kazi ya Kamati tutakwenda katika maeneo husika yote yenye migogoro na tutashirikisha wawakilishi wa wananchi, wakiwemo Wabunge na Madiwani, kuhakikisha kwamba eneo tutakaloliwekea mipaka halitakuwa na migogoro tena. (*Makofi*)

SPIKA: Muda hauko upande wetu. Sasa nipitie matangzo kidogo, niweke meza yangu hapa iwe safi.

Wageni walipo Bungeni leo tuna wageni muhimu na maarufu. Naomba ningeomba Waheshimiwa Wabunge, hebu wanaotembea tembea tukae na tusikilizane kidogo.

Ninao wageni wengi kidogo wa katika Jukwaa la Spika na ningeomba niwatambulisha vizuri. Kama nilivyowaambia kabla, tuna ujumbe maalum kutoka kwenye mabunge mbalimbali ambao tunao leo kama wageni wetu, lakini pia wageni hao ambao baadhi yao ni Maspika kutoka Mabunge ya kutoka nchi za Misri, Burundi na Cameroon. Tunamwona Mheshimiwa Naibu Spika yuko nao pale kama mwenyeji wao. *(Makofi)*

Naomba kwanza nimtambulisha Spika wa Bunge la Misri, Dkt. Ali Abdel Alal Sayyed Ahmed, karibu sana Spika wa nchi rafiki ya Misri, karibu sana Tanzania, karibu Dodoma tunafurahi sana kuwa nawe miongoni mwetu na Spika huyu ameniambia yeye ni shabiki wa timu ya Al Ahly. Nikamwambia na mimi ni shabiki wa timu fulani, tumekuchapa bao moja. *(Makofi)*

Tunaye Balozi wa Misri nchini Tanzania Mheshimiwa Mohamed Gaber Abulwafa, karibu sana Mheshimiwa Balozi. *(Makofi)*

Tunaye pia Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya Afrika kutoka huko huko Mheshimiwa Tarek Tadwan. Pia tunaye Katibu wa Bunge la Misri Ndugu Kansela Saadeldin. *(Makofi)*

Tuna baadhi ya Wabunge ambao wamefuatana na Mheshimiwa Spika akiwemo Fawyz Abozereba, lakini pia tunaye Mbunge Mheshimiwa Maged Abouelkhir, tunaye pia Mkuu wa Sekta katika Bunge la Misri Alaa Edin Nagy, lakini Mkuu wa Usalama katika Bunge la Misri Meja Mohamed Elmagharabi na Msaidizi wa Mheshimiwa Spika, Kapteni Mohamed Elahmady, eeh hii sasa hii, ahsanteni sana. *(Makofi/Kicheko)*

Tunawashukuru sana na kuwakaribisha ujumbe wa Misri na baadae kidogo nitawatangazia Waheshimiwa Wabunge

itabidi tukutane na Waheshimiwa Maspika hawa katika Ukumbi wa Pius Msekwa tupate kusikia wakizungumza na sisi. *(Makofi)*

Pia tuna heshima ya kuwa na ujumbe wa Spika na Wabunge kutoka nchi jirani ya Burundi wakiongozwa na Rais wa Seneti ya Burundi, Mheshimiwa Reverin Ndikuriyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Burundi wana Mabunge mawili; Bunge la Juu na la Chini kwa maneno ya kawaida, sasa la juu lile ndiyo Seneti ambalo sasa Spika wake ndio Mheshimiwa Ndikuriyo na niongeze kusema kwamba Maspika hawa wawili; Spika wa Misri na Spika wa Burundi pamoja kwamba ni Maspika pia ni Makamu wa Rais wa nchi zao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunaye Balozi wa Burundi nchini Tanzania Mheshimiwa Gervais Abayeho, lakini pia Mheshimiwa Spika wa Burundi amekuja na Mheshimiwa Naibu Spika wa Kwanza Ndugu Georges Nshimirimana, lakini pia amefuatana na Naibu Spika wa Pili Mheshimiwa Domitien Bavakure. *(Makofi)*

Pia amefuatana na Maseneta wawili, Mheshimiwa Jean Chubwa, Seneta mmojawapo, Seneta mwingine ni Mheshimiwa Veneranda Nizigiyimana. Ahsante sana. *(Makofi)*

Lakini pia amefuatana na Wakuu wa Mikoa watatu wao wanawaita Magavana, kwa hiyo amaefuatana na Magavana watatu; wa kwanza ni Gad Niyukuri, mwingine ni Aline Manibarusha na Gavana mwingine ni Fidele Minani. Magavana hawa wanatoka Mikoa ambayo inapakana na Tanzania. *(Makofi)*

Lakini pia yupo na Mkuu wa Utawala katika Seneti - Erick Nkuruzimana. Lakini pia yupo Afisa Itifaki wa Seneti - Louise Mbonipa pamoja na Afisa Habari wa Seneti - Pascasie Hatungimana na Afisa Habari mwingine wa Seneti Oliva Nindamutsa. Karibuni sana ujumbe mzima wa Spika wa Burundi pamoja na maafisa uliofatana nao. *(Makofi)*

Pia upo ujumbe wa kutoka *Commonwealth Parliamentary Association (CPA)* ambapo tunaye Naibu Spika wa Bunge la Cameroon ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji ya Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola, Kimataifa (*CPA-International*) na kwa hiyo huyu ndiye Rais wa *CPA-International* Mheshimiwa Emilia Lifaka. Karibu sana Emilia. (*Makofi*)

Huyu ni mgeni wetu, lakini pia ni mgeni maalum wa *CPA-Tanzania* na ni mgeni wa *TWPG*. Lakini pia amefuatana na msaidizi wake ambaye ni Ndugu Beatrice Ikome. Karibu sana Beatrice. (*Makofi*)

Tuna wageni saba wa Mheshimiwa Spika waliotoka katika Taasisi ya Kimataifa na Vyombo vya Habari (*International Press Institute - IPI*) wakiambatana na viongozi wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (*TEF*) wakiwa na Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Ndugu Deodatus Balile; yupo pia Katibu wa Jukwaa la Wahariri Ndugu Neville Meena; Naibu Mkurugenzi wa *IPI* Ndugu Scott Griffen; yupo Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya *IPI* Ndugu Khadija Patel; yupo Mjumbe wa Bodi ya *IPI* Ndugu Carsten Von Nahmen; yupo Mshauri Mkuu wa Masuala ya Kisheria wa *IPI* Ndugu Ravi Prasad na Mjumbe wa *IPI* Ndugu Jokine Matilda. (*Makofi*)

Wageni wengine ni wa Waheshimiwa Wabunge nao ni wageni wa Mheshimiwa *Engineer* Edwin Ngonyani ambaye ni mtoto wake kutoka Kigamboni, Dar es Salaam Ndugu Kakayeka Ngonyani. Kakayeka yupo kule. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni ndugu zake kutoka Tukuyu Mkoani Mbeya wakiongozwa na Ndugu Elizabeth Mwakalasya. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa James Ole Millya ambao ni wapiga kura wake na wawekezaji kutoka Jijini Arusha, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo Mererani, Ndugu Adam Kobelo. Karibu sana. (*Makofi*)

Lakini pia ninaye Mwenyekiti wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Dodoma ambaye yupo miongoni mwetu Ndugu Billy Francis Chidabwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nadhani wageni wameisha.

MBUNGE FULANI: Bado.

SPIKA: Yupo mgeni mmoja kwa kweli simfahamu, huyo naomba nimpe heshima Mheshimiwa Mariam Ditopile atumie dakika moja kumtambulisha mgeni huyu, simfahamu vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mariam tafadhali.

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Spika, nashukuru na kama inavyofahamika mimi ni Mbunge wa Vijana na kwa mujibu wa nchi yetu ujana ni mpana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mgeni wa mwisho kutambulishwa jina lake ni Peter Mollel almaarufu *Pierre Liquid*, huyu ni Mtanzania mzalendo, mjasiriamili wa *furniture* anayepatikana Chang'ombe, Jijini Dar es Salaam lakini baada ya kazi Ndugu Pierre ni mpenda burudani na ana kijiwe chake kinaitwa *Liquid* na ndio maana umaarufu yake *Pierre Liquid*. Lakini katika kupata burudani yake hivi karibuni ametoka kupata umaarufu wa hali ya juu sio tu kwa nchi yetu lakini hata nje ya mipaka ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umaarufu huu ni kutokana na sanaa ya vichekesho. Ndugu Pierre ni maarufu kwa kauli zake ambazo huwafurahisha watu na hata kama una msongo wa mawazo unasahau, hakika Mheshimiwa Spika, utabaki kileleni, utazidi kuwa juu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini mzalendo huu kutokana na kipaji chake ambacho tumeona kina Mzee Majuto leo hii tunamuenzi kutokana na kipaji cha vichekesho, lakini kuna Mr. Bean ambaye amekuwa tajiri bilionea kutokana na kipaji hiki cha vichekesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Ndugu Pierre Liquid ametoa mchango wake ni kati ya watu ambao walijitoa mhanga kuleta hamasa na ikafanikisha ushindi mnono wa tatu bila kwa *Taifa Stars* kubaki kileleni hadi Misri. (*Makofi*)

Kwa hiyo, napenda kumalizia, Ndugu Peirre Liquid anasadifu maneno ya wahenga wanaosema Mungu akitaka kupa hakuandikii barua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Timu yetu ya Taifa itakwenda kushiriki mashindano ya Afrika kule Misri, kule Cairo, Alexandria namwambia Mheshimiwa Spika wa Misri tunakuja huko. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Ndugu Pierre karibu sana. Mimi kwa kweli nilikuwa simfahamu basi niseme karibu sana Bungeni, Magufuli utabaki kuwa juu, utabaki kileleni. (*Makofi/Kicheko*)

Ndugu Pierre Wabunge hawajakuona, upo wapi Pierre? Karibu sana mjengoni. Karibu sana *konki fire*. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa nina matangazo madogo ya kumalizia. Tangazo la Mheshimiwa Shally Raymond, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Moore hapa Bungeni....

Naomba tulikilizane, leo Jumatano tarehe 3 Aprili, 2019 kutakuwa na ibada ya misa kwa Wakristo Wakatoliki mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge saa saba mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa, ghorofa ya pili. Wakatoliki kuna ibada jengo la Pius Msekwa, ghorofa ya pili, Mheshimiwa Shally Raymond anawaomba mkutane pale.

Lakini pia naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge mara tu tukimaliza shughuli zetu hapa, wote kabisa tuelekee Ukumbi wa Msekwa ambapo tutapata *goodwill messages* kutoka kwa wageni wetu maarufu ambao tumewapa leo, nawaomba sana tukitoka hapa tupate chai

ya haraka haraka tuelekee Ukumbi wa Msekwa wote ambapo tutapata mazungumzo maalum na wageni wetu leo. (*Makofi*)

Pia nawaomba watumishi wa Bunge wale ambao mpo leo muwepo Msekwa pia ili tuweze kuwasikiliza wageni wetu, wageni hawa ni wa Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge wote pia mnakaribishwa pale Msekwa. (*Makofi*)

Mwisho, jana palijitokeza sintofahamu kidogo, nafikiri wote mlikuwepo, kwa hiyo hamhitaji kusimuliwa, Mheshimiwa Lema alijilipua, kwa hiyo suala lake naagiza liende katika Kamati ya Maadili kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Spika alikwishafanya jana na Kamati hii ya Maadili ikutane kuanzia saa nane leo mchana na suala lake liishie leo leo, ikiwezekana mambo yake kesho yawe yamekamilika.

Kwa hiyo, Kamati ya Maadili saa nane kamili mchana muanze kikao, Mheshimiwa Lema kuanzia saa saba uwe katika maeneo yale ili uweze ku...

MHE. GODBLESS J. LEMA: (*Hapa hakutumia kipaza sauti*).

SPIKA: Ndiyo uende huko, maana ulisema huogopi, na mimi niliwaambia Waheshimiwa Wabunge, Spika Ndugai haogopi pia, kabisa. Wanaofikiri sisi dhaifu, sisi sio dhaifu, nilishasema na nikarudia na nikarudia, yeyote ambaye anataka kuingia kwenye kumi na nane hiyo sisi tupo tayari na yeye huyo. Hizi ni *procedures* tu, lazima tutawapeleka huko, kwenye Kamati ile ambayo baadhi walisema kwamba ina udhaifu fulani, basi Mheshimiwa Lema atakwenda huko na kesho panapo majaaliwa, tutaifahamu hatima yake. Mwingine anayejiona na yeye, anaalikwa kwenye mchezo huo, kabisa kabisa, yaani nataka sasa tuthibitisha Bunge hili la Kumi na Moja kweli lina uongozi na tutathibitisha, hatumwogopi yeyote. (*Kicheko*)

Pia niwaambie wananchi mambo haya wanayoyaona, mambo mengine hawayaelewi vizuri, ipo misongo mingi sana

ya mawazo humu ndani, labda ndiyo inasababisha mambo haya, maana ninyi ni wawakilishi wa wananchi, unapokuja hapa lazima uwakumbuke wale watu unaowawakilisha kule waliokutuma hapa, ukitanguliza *personal interest*, ukisema mimi siogopi, sio wewe ni wale unaowawakilisha hapa, wana haki ya wewe kuwawakilisha hapa.

Kwa hiyo, wakati mwingine kati ya wewe na wale lazima upime kipaumbele ni nani, ukiweka kipaumbele wewe, kidogo hapo inakuwa siyo sawasawa sana. Kwa hiyo wakati mwingine hapa watu wana msongo wa mawazo. Kwa mfano, yapo mambo huwa hatusemi, lakini lazima niseme kidogo, Mheshimiwa Lema tangu aje hapa Bungeni amekopa shilingi milioni 644.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Useme aaaa, useme eeee, ndiyo hivyo, nimekuona Mheshimiwa Esther Matiko toka nje, kusanya vitu vyako toka nje, sasa hivi.

(Hapa Mhe. Esther N. Matiko alitoka Ukumbini)

SPIKA: ...shilingi milioni 644, ameshalipa lipa sasa hivi anadaiwa shilingi milioni 419, huo ni msongo wa mawazo ndiyo maana mtu anafika mahali anaweza akajilipua tu.

Sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 4:35 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 4 Aprili, 2019 Saa Tatu Asubuhi)